

NGURUMO 1/12/12

Kiongozi wa FRELIMO

katiwa ndani

Organising Secretary wa FRELIMO, Moshi, Bw. Inasio Minga katiwa ndani kwa ajili ya kutumia fedha za Chama, kwa njia zisizo halali. Mkaaguzi wa chama hicho, Bw. A. S. Camando, alipofika Moshi majuzi akiwa katika kutembelea ofisi zote za Frelimo kwa ukaguzi wa fedha, aligundua kwamba kadi 3 zenye thamani ya Shs 10/50 hakuna Bw. Camando alipozidi kuchungua zaidi aligundua tena kuna kadi nyingine 6 zilizouzwa na Bw. Minga wakati alipokuwa Tanga, na fedha zile kadiri ya shs 21/- na akazitia kibindoni!!

Bw. Minga alipoulizwa kama ni kweli au vipi, alikataa kukutuu akisema hakuuza hata kadi moja kwa mkono wake, pia hakula hata senti moja ya chama. Lakini baada ya uchunguzi, zikapatikana kadi nne zilizokuwa na sahihi ya Bw. Minga! hapo tena jamaa wakapata kizibiti, na bila kukawia wakampeleka polisi. Kesi bado lakini yupo ndani.